Maisha, Kifo na Ufufuo wa Kristo

“Katika maisha ya Kristo ya utii kamili kwa mapenzi ya Mungu, mateso yake, kifo chake na ufufuo, Mungu aliandaa tayari njia pekee ya upatanisho kwa dhambi ya mwanadamu, ili kwamba wale ambao kwa imani watapokea upatanisho huu wapate uzima wa milele, na ulimwengu wote uweze kuelewa vema upendo mtakatifu usio na kikomo wa Muumbaji. Kafara hii kamilifu huthibitisha haki ya sheria ya Mungu na neema ya tabia yake; kwa sababu hufanya vyote kuhukumu dhambi yetu na kutoa njia ya msamaha wetu. Kifo cha Kristo ni badala na hufidia, kikipatanisha na kubadilisha. Ufufuo wa Kristo hutangaza ushindi wa Mungu dhidi ya majeshi ya uovu, na kwa wale wanaipokea kafara hiyo huhakikishiwa ushindi hatimaye dhidi ya dhambi na mauti. Inatangaza ukuu wa Yesu Kristo ambaye mbele zake kila goti mbinguni na duniani litapigwa. (Yoh.3:16; Isa.53; 1Pet.2:21, 22; 1Kor.15:3, 4, 20-22; 2Kor.5:14, 15, 9-21; Rum.1:4; 3:25; 8:3, 4; 1Yoh.2:2; 4:10; Kol.2:15; Filp. 2:6-11)” Msingi wa Imani kutoka Kanuni za Kanisa.

Katika Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, baada ya ibada (Uf. 4:11), Yohana aliona kwenye mkono wa kuume, kuna kitabu kilichoandikwa ndani na nyuma, kimetiwa muhuri saba (Uf. 5:1). Malaika mwenye nguvu akahubiri, ni nani astahiliye kukifungua kitabu na kuvunja mihuri yake? (Uf. 5.2). Hapakupatikana mwenye kustahili kufungua wala kukitazama. Yohana akaanza kulia. Lakini Malaika akamwambia usilie (Uf. 5:5). Baadaye Yohana anamwona Mwanakondoo na huyo akaabudiwa (Uf. 5:13). Miaka mingi kabla hajazaliwa Mwanakondoo alisema tazama nimekuja, kuyafanya mapenzi yako eh Mungu wangu ndiyo furaha yangu (Zab. 40:7, 8). Kuja kwa Mwanakondoo aliyechinjwa kabla haijawekwa misingi ya ulimwengu (Uf. 13:8) kulimkomboa mwanadamu.

Neema ya Mungu iokoayo

Maandiko humfunua Mungu mwenye kujali wanadamu (Yoh. 3:16). Mungu ni pendo (1 Yoh. 4:8), humfikia mwanadamu kwa upendo wa milele (Yer. 31:3). Anapotualika, hutuachia uhuru wa kuchagua (Uf. 3:20, 21). Matumizi ya nguvu ni kinyume na utaratibu wa Mungu.

Neema inaanzia kwa Mungu Mwanadamu alipokosa, Mungu alitangaza uadui baina ya uzao wa nyoka na uzao wa mwanamke. (Mwa. 3:15).

Neema na Haki. Neema imejichanganya na haki kwa namna ya ajabu (Kut. 34:6, 7; Zab. 85:10)

Kusamehe au kuadhibu?

Katika uasi wa Israeli, Mungu alisihi wanadamu waungame wamrudie (Yer. 3: 12 - 14). Hata hivyo walikataa (Yer. 5:3). Roho isiyoungama, hulazimisha adhabu isikwepeke (Zab.7: 11, 12). Japo Mungu ni mwenye rehema, hatawasamehe wanaong’ang’ania dhambi (Yer. 5:7). Msamaha una makusudi. Mungu anakusudia kuwabadilisha wadhambi kuwa watakatifu. (Isa. 55: 7). Ujumbe wake ni unasikika kila kona, niangalieni mkaokolewe enyi ncha za dunia (Isa. 45:22)

Ghadhabu ya Mungu dhidi ya Dhambi

Anguko la awali lilimfanya mwanadamu awe na uadui na Mungu (Kol. 1:21). Hivyo tulistahili ghadhabu ya Mungu ambaye ni moto ulao (Ebr. 12:29, Hab. 1:13). Ukweli ni kwamba wote

tumefanya dhambi (Rum. 3:23), na kwa asili ni wana ghadhabu (Efe. 2:3, cf. 5:6) na kustahili kifo kwa kuwa mshahara wa dhambi ni mauti. (Rum. 3:26). Ghadhabu ya Mungu ni itikio la Mungu kwa dhambi (Rum. 1:18). Kumkataa Mungu kwa makusudi huamsha ghadhabu yake (2 Falme 17:16-18, 2Nyak.36:16). Mungu huchukia dhambi na utukufu wake huichoma, hata hivyo Mungu anapenda ulimwengu uokolewe, hivyo anamjali kila mdhambi.

Mwitikio wa Mwanadamu

Jinsi Mungu alivyoshughulika na Israeli, inatupatia ufahamu juu ya wingi wa neema yake upitao kiasi. (Efe.2:7). Yohana anasema tuliona utukufu wake mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli. (Yoh. 1:7). Yesu amefanywa hekima kwetu, ili kila aonaye fahari, na aone fahari juu ya Bwana. (1Kor. 1:30, 31). Ni nani atakayedharau wingi wa wema, ustahimilivu na uvumilivu wake, ambao unatuvuta tupate kutubu? (Rum. 2:4). Hata mwitikio wa mwanadamu kwa wema wa Mungu hauanzii kwa mwanadamu mwenyewe bali kwa Mungu (Rum. 12:3), hata toba yatoka kwake (Mdo. 5:31). Upendo wetu huamshwa kuitikia alivyotupenda kwanza (1 Yoh. 4:19). Hatuwezi kujiokoa (Yer. 13:23, Yoh. 15:5). Haki yetu wenyewe ni sawa na nguo iliyotiwa unajisi (Isa. 64.6). Ametufanya kuwa hai katika Kristo, kwa kuwa tumeokolewa na neema yake kwa imani, ni karama ya Mungu (Efe. 2: 4, 5, 8, 9)

Huduma ya Yesu ya Upatanisho

Habari njema ni kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake (1 Kor. 5:19). Tumepatanishwa na Mungu kwa mauti ya Kristo (Rum. 5:10). Sasa tunashangilia kwa kuwa tumepokea huo upatanisho (Rum. 5:11). Kafara ina nguvu kulipia maovu, lakini lazima Kuhani ahudumu (Law. 4:20, 26, 35, Law. 16:15-18, 32, 33). Hivyo, kwa kifo na huduma yake ya ukuhani upatanisho hukamiliswa.

Kafara ya Yesu ya Upatanisho. Mungu aliupatanisha ulimwengu na nafsi yake kwa njia ya Yesu Kristo (1 Kor. 5:19). Siyo kwamba Mungu hataadhibu au kwamba ghadhabu yake dhidi ya dhambi imekoma, bali imepatikana njia ya kumsamehe mwenye dhambi anayetubu wakati madai ya haki ya sheria yake yakiwa yametimizwa.

Umuhimu wa Kifo cha Yesu.Kwa Mungu mwenye haki kudumisha haki yake, kifo cha Yesu kilikuwa muhimu kimaadili na kisheria. Alionyesha haki yake, na aweza kwa hicho kumhesabia haki amwaminiye. (Rum. 3:25, 26)

Kafara ya upatanisho yaweza kukamilisha nini? Ni Mungu mwenyewe ndiye aliyemtoa mwanawe awe kafara ya upatanisho (Rum. 3:25). Kifo cha Yesu ni toleo la Mungu lenye harufu ya manukato (Efe. 5:2 cf. Mwa. 8:21 Kut. 29;18 Law. 1:9). Kafara imeondoa kizuizi cha mwanadamu mwenye dhambi kumfikia Mungu.

Kristo Mbeba dhambi badala ya Wanadamu. Mungu aliridhika kumchubua, na kwake yaliwekwa, maovu yetu sisi sote (Isa. 53: 5, 6, 10, 12 cf. Gal. 4:4). Kristo alikufa kwa dhambi zetu kama yanenavyo maandiko (1Kor. 15:3). Dhambi zilizotuchafua zikihamishiwa kwa Yesu, sisi tunatakasika (Zab. 51:10).

Nini umuhimu wa damu? Damu ndiyo uhai, ambao umetolewa kuwa upatanisho wa dhambi zetu (Law. 17:11). Damu ya Yesu ni bora kuliko ya wanyama na hutakasa kabisa (Ebr. 9:14). Kumwagika damu yake, kulitupatia upatanisho (Rum. 3:25; 1Yoh. 4:10)

Yesu fidia. Wanadamu walipokuwa chini ya utawala wa dhambi, walihukumiwa kulaaniwa na sheria ya Mungu (Rum. 6:4, Gal. 3:10 – 13). Wakiwa watumwa wa dhambi (Rum. 6:17), walikuwa watu wanaostahili kifo (Rum. 6;23). Hakuna mwanadamu ambaye angetoa fidia kwa nafsi yake (Zab. 49:7). Ni Mungu tu mwenye uwezo wa kukomboa na kaburi (Hos. 13:14). Yesu hakuja kutumikiwa bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia kwa wengi (Mt. 20:28 1Tim. 2:6). Amelinunua Kanisa kwa damu yake (Mdo. 20:28). Kwa Yesu tuna ukombozi…msamaha wa dhambi. (Efe.1:17; Rum. 3:24). Kifo chake ni kutukomboa na maasi yote, kujisafishia watu wenye juhudi katika kutenda mema (Tit. 2:14).

Fidia imekamilisha nini? Fidia imemrudishia Mungu miliki ya mwanadamu (1Kor. 6:19, 20; 1Kor.7:23). Tumekombolewa tuondokane na mwenendo usiofaa tuliorithi (1Pet. 1::18). Tunawekwa mbali na dhambi, tunatakaswa na kupata uzima wa milele (Rum. 6:22). Tunakuwa ufalme wa makuhani (Uf. 5:9, 10)

Yesu mwakilishi wa Wanadamu. Adamu wawili (Adamu na Kristo 1Kor. 15:45,47)) ni wawakilishi wa wanadamu. Katika Adamu wanadamu walikufa, katika Kristo, wanahuishwa (1Kor. 15:22). Kifo cha Yesu kimeleta upatanisho na uzima kwa mdhambi mwenye kutubu (2Kor. 5:21, Rum.6:23, 1Pet. 3:18). Kwa kila mtu, alionja mauti (Ebr. 2:9). Kwa Adamu wote walikosa (Rum. 5:12). Mauti inayosemwa hapa tuliyolipiwa na Yesu ni ile ya pili (Uf. 20:6)

Maisha ya Yesu na Wokovu

Ilichukua maisha ya Yesu na kifo chake kuziba shimo la dhambi (Rum. 5:10)

Maisha ya Yesu yanatufanyia nini? Maisha yake matakatifu yanahesabika kuwa vazi la arusi (Mt. 22:11), au vazi la haki (Isa. 61:10). Hilo ndilo tunalopewa ili tuondokane na nguo iliyotiwa unajisi (Isa.64:6). Kuja kwetu kanisani, au kuitikia mwaliko hakutoshi (Mt. 22:10), twapaswa kuwa wenye kuonyesha kwamba tumekombolewa na Yesu (Mt. 22:13).

Maisha ya Yesu yanatutia moyo

Maisha ya Yesu ni kielelezo ya jinsi tunavyopaswa kuishi. Tukitwezwa, tuvumilie (1Pet. 2: 21-23). Yesu hutoa uhakika kwamba kwake yeye tu washindi (Wafil. 4:13).

Ufufuo wa Yesu na Wokovu

Kama Yesu asingefufuka, kuhubiri ni bure, imani ni bure, bado wanadamu tungalimo dhambini (1Kor. 15:14,17) Yesu alifufuka na mwili aliokufa nao (Luk. 24:36-43). Alipaa akaanza kazi ya upatanisho kwenye mkono wa kuume wa Mungu (Ebr. 8:1).

Kwa nini Yesu alikuja mara ya Kwanza?

Kujifunza kwa makini Agano Jipya kunadhihirisha kwamba kulikuwepo makusudi ya Yesu kuja duniani. Siyo kwamba alikuja kwa bahati mbaya. Mara nyingi alisema alikuja kwa kutumwa na Baba yake (Luk. 2:49, 4:43, 9:22, 24:44). Alijua kwamba yeye ni Mwana aliyetumwa (Mk. 12:6, 7). Baba alimtakasa akamtuma (Yoh. 10:36), akampa mamlaka (Yoh. 8:42 Mt. 9:6). Haikuwa kwenye mamlaka yake kutenda atendayo (Yoh. 4:34, 5:30, 6:38). Baadhi ya makusudi ya Yesu kuja ulimwenguni yameelezwa kwenye Maandiko.

Kazi gani Yesu alikuja kuifanya?

1. ***Kuthibitisha Ahadi za Mungu.*** Alifanyika mwili kuthibitisha ahadi zilizotolewa na Mungu kuanzia na ile ya uadui wa uzao wa nyoka na uzao wa mwanamke (Mwa. 3:15) na kuendelea kwenye sehemu zingine za agano la kale (Isa. 7:14, 9:6, Mika 5:2). Ujio wake kama dhabihu ulitabiriwa na kafara za Agano la Kale (Mwa. 4:3, Walawi 1:3-9, 17:11) na kutangazwa na manabii (Isa.52:13, 14, 53:3-6, Dan. 9:26, Zek. 13:1, 7) na Mfalme wa Ufalme wake (Mwa. 49:9, 10, Zab. 2, Yer. 23:5, 6)

2. ***Kuanzisha Ufalme wa Mungu.*** Ni dhahiri Yesu alikuja kutambulisha mamlaka isiyo na kikomo ya Mungu na kuanzisha ufalme wake (Mt. 4:17, Luk. 19:11-27). Wakati akihudumu, wako waliofikiri Ufalme wa Mungu ni jambo la wakati ujao, kumbe ufalme wa Mungu ulikuwako hapohapo pamoja nao (Mt. 12:28). Siri ya kuwa sehemu ya ufalme wa Mungu ni kukubali kuwa sehemu yake tangu sasa Mt. 7:23, 25:41).

3. ***Kutoa elimu ya Mungu.*** Kwa kuwa kumjua Mungu ni jambo la wokovu, Yesu alikuja ili tumjue Mungu (Yoh. 17:3), Kwenye Agano la Kale Mungu alijulikana kama Muumbaji na Mtawala (Zab. 33:6, 9, Isa. 40:12 – 17, 45:18) na siyo sana kama Baba wa taifa lililokombolewa (kama Kumb. 32:6, Isa. 22:21, 63:16, Mal. 1:6) Yesu alisaidia wenye dhambi kumfikiria Mungu kwa upendo na utisho, asiyezuilia chema kwa watoto wake. Ufunuo huu ungewezekana tu kwa njia ya Yesu (Mt. 11:27, Luk. 10:22) kwa matendo yake zaidi ya mafundisho yake kwa kuwa Baba alikuwa ndani yake (Yoh. 14:7-14)

4. ***Kuwa Mtumishi wa Mungu.*** Yesu alidai hakuja kutumikiwa bali kutumika (Mt. 20:28). Wazo la kuwa mtumishi wa Mungu liko kwenye mashairi yaliyoko kwenye kitabu cha Isaya (Isa.42:1-4, 49:1-6, 50:4-9, 52:13-53:12). Japo imejadiliwa, yeye ni Mtiwa mafuta wa Mungu (Isa. 42:1) kuanzisha haki (mafungu ya 1,3,4), kufikisha utumishi kwa mataifa (fungu la 1, 4 na Isa. 50:4) na Israeli (Isa.49:5, 6a), mwenye kuwezesha wokovu wa Mungu ufikie wanadamu (Isa. 49:1-6), kutimiza yote haya kwa kujitolea (Isa.53:4-6, 8 10-12). Neno aliyekuwa sawa na Mungu (Wafil. 2:6) alichukua hadhi ya mtumishi (mafungu ya 5-7).

5. ***Kuishi maisha kielelezo kwa wanadamu.*** Kwa lugha ya mfano, chakula chake kilikuwa kuyafanya mapenzi ya Baba yake (Yoh. 4:34). Hakuja duniani kufanya mapenzi yake (Yoh. 6:39, cf. 5:30). Akitofautiana na Adamu wa kwanza, yeye alitii mapenzi ya Baba yake hata alipokuwa akiteswa (Ebr. 5:8, 9 Mt. 26:39-45, Luk.22:42-46)). Tumeitwa kufanana naye (Rum. 8:29), kumvaa na kutotegemea matendo ya mwili (Rum. 13:14, cf Kol. 3:10) kumwiga (1Thes. 1:6) kuenenda kama alivyoenenda (1 Yoh. 2:6) hata kama tukiteswa (1 Pet. 2:21)

6. ***Kuwaponya wadhaifu na wagonjwa.*** Aliponya wengi (Mt. 4:23), alipotembelea vijiji, miji na maeneo ya sokoni (Mk. 6:56 cf. Luk. 4:40). Walimfuata makutano mengi kuponywa magonjwa yao (Luk. 5:15), uwezo wa Bwana ulikuwako kuponya (fungu la 17). Hata mitume kwenye utume wao walipewa mamlaka kuponya (Mt.10:5-8 cf Luk. 10:8, 9). Yesu aliona magonjwa kama matokeo ya dhambi alizokuja kutuondelea (Mt. 8:17, Isa.53:4). Kwa hiyo kuponya ilikuwa sehemu ya kutekeleza mpango wa Mungu kwa wanadamu.

7. ***Kuifanya dhambi iwe mbaya kabisa.*** Katika mpango wa Yesu wa neema, ilikuwa kudhihirisha jinsi uadilifu wa mwanadamu usivyotosheleza. Mafundisho yake yalifanya dhambi ionekane mbaya kabisa na kuwepo kwake, kulifanya watu wajisikie wadhambi (Luk.5:8, 7: 36-50). Yeye aliyemshinda mwovu (Mt.4:1-11 Yoh. 16:33) wadhambi waovu walimwua na kudhihirisha hatia na hitaji la mwanadamu.

8. ***Kuwa Kuhani Mkuu.*** Alikuja apate sifa ya kuwa Kuhani Mkuu kwa kupitia uzoefu wa kibinadamu (Ebr. 2:17, 18). Alifanya kazi ya Kuhani Mkuu kwa mambo matatu: kwanza kutoa kafara ya mwaka, pili: upatanisho kwa ajili ya watakatifu na tatu: kubariki watu (Law. 4:16-21, Law. 16:1-28)

9. ***Kuokoa wanadamu kwa kifo chake.*** Utume wa Yesu ulihusisha kifo chake. Alikuja kuzivunja kazi za mwovu (1Yoh. 3:8) na kuziondoa dhambi (fungu la 5,) hivyo kuwaokoa kabisa wale walioishi wakiwa watumwa wa uovu (Ebr. 2:14, 15). Alikuja kuokoa wadhambi (1 Tim. 1:15, Mt. 1:23,21). Ili kuokoa mwenye dhambi, kifo cha Yesu ni muhimu (1Tim. 2:14).

Matokeo ya Huduma ya Yesu ya Wokovu

Matokeo ya kafara ya Yesu hayagusi tu wanadamu bali pia ulimwengu wote.

Upatanisho wa Ulimwengu

Ukombozi ndani na kupitia kanisa ni mkubwa. Hekima ya Mungu ijulikane, katika ulimwengu wa roho (Efe. 3:10). Ulimwengu umepatanishwa na Nafsi ya Mungu (Kol. 1:20). Kila goti, mbinguni, duniani na majini lapaswa kupigwa kwa Yesu (Wafil. 2:10, 11)

Sheria ya Mungu imetukuzwa

Aliihukumu dhambi katika mwili na madai ya sheria yapate kutimizwa kwetu siisi katika roho (Rum. 8:3, 4)

Kuhesabiwa haki

Mwana aliyepotea alipatanishwa na baba yake baada ya kuupokea upendo na msamaha wa baba yake. Mungu hutupatia kuhesabiwa haki (Rum. 5:1). Siyo tena wanaokabiliwa na ghadhabu ya Mungu bali wana wapendwa ambao kuvunja vipingamizi vilivyowakilishwa na uadui baina na Wayahudi na Mataifa (Efe. 2;14-16)

Ubatili wa matendo katika kuleta Wokovu

Kwamba Mungu anahudumu kwa wokovu (Yoh. 3;16) kuupatanisha ulimwengu na nafsi yake(1 Kor. 5:19), kuanzisha na kukamilisha imani yetu, (Ebr. 12:2) huonyesha juhudi ya mwanadamu hata iweje, hawezi kujiokoa (Yer. 13;23). Shukrani ya waliopokea msamaha, hufanya watu wampende Mungu na utii kuwa jambo la furaha (Yoh. 14;15), wala siyo njia ya wokovu (Rum. 3:20).

Mahusiano Mapya na Mungu

Kupokea neema ya Mungu, ambayo humpatia mwanadamu maisha makamilifu ya Kristo, haki yake, kifo cha upatanisho huongoza kwenye mahusiano makini na Mungu yasiyo ya hofu. (Yoh. 15: 1-10)

Hututia shime kuhubiri

Upendo wa ajabu wa Mungu uliodhihiriswa na huduma ya Mungu ya upatanisho kwa njia ya Yesu Kristo hututia shime kuwaalika wengine nao waishiriki. Hatutanyamaza. Kwa vinywa vyetu tutasihi wengine wapatanishwe na Mungu (2Kor. 5:20, 21).